

**OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA SUMBAWANGA**

SHULE YA SEKONDARI KIKWALE,
S.L.P 105,
SUMBAWANGA.

TAREHE

JINA LA MWANAFUNZI
S.L.P 229
SUMBAWANGA.

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021

1. UTANGULIZI

Ninayo furaha kukujulisha kwamba umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza mwaka 2021 katika shule ya Sekondari Kikwale iliyopo Kata ya Mfinga umbali wa kilometa 77 toka makao makuu ya Wilaya ya Sumbawanga.

Usafiri wa basi toka Mjini Sumbawanga unapatikana katika kituo cha mabasi kilichopo Mjini Sumbawanga kwa Tsh. 8000/=

Unatakiwa kuripoti shuleni siku ya ~~ITUMAA~~ tarehe 08/01/2021 bila kukosa

**2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA
SARE ZA SHULE.**

WASICHANA

- a. Sketi mbili, moja kijani jeshi na nyingine Khaki
- b. Masha ti mawili meupe mikono mifupi
- c. Tai mbili, moja kijani jeshi na nyingine Khaki
- d. Soksi ndefu nyeupe pea mbili au zaidi
- e. Vazi la kujikinga na baridi, sweta la kijani jeshi lisilo na maandishi
- f. Viatu vya ngozi pea mbili vyeusi vya kisigino kifupi vya kamba
- g. Raba za michezo na track suti rangi yoyote
- h. Hijabu kitambaa cheupe (kwa waislamu tu)
- i. Tshirt ya shule rangi ya kijani jeshi

WAVULANA


- a. Suruali mbili, moja kijani jeshi na nyingine Khaki
- b. Mashati mawili meupe mikono mifupi
- c. Tai mbili, moja kijani jeshi na nyingine Khaki
- d. Soksi ndefu nyeusi pea mbili au zaidi
- e. Vazi la kujikinga na baridi, sweta la kijani lisilo na maandishi
- f. Viatu vya ngozi pea mbili rangi nyeusi vya kisigino chenye Soli fupi vya kamba (siyo buti)
- g. Raba za michezo na track suti rangi yeyote
- h. Tshirt ya shule rangi ya kijani jeshi
- i. Mkanda mweusi wa ngozi

MAMBO MENGINE MUHIMU UNAYOTAKIWA KUKAMILISHA

- i. Unatakiwa uje na daftari Counter book Q3 Dazani moja ambayo ni sawa na daftari 12, Mathematical set moja, Rula Moja , Kalamu za blue au nyeusi za kutosha na penseli.
- ii. Picha mbili za passport size (andika jina lako nyuma)
- iii. Uje na Tembe lenye mpini au fyekeo kwa ajili ya usafi

NB: Shule hii inaongozwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu namba 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebisha kwa sheria namba 10 ya mwaka 1995. Pia inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara husika. Utapewa nakala mara baada ya kusomewa na kupata ufafanuzi wa kila kipengele cha sheria mara baada ya kufika shuleni. Usije na simu ya mkononi. Hairuhusiwi

Mwisho, Ninakutakia maandalizi mema, Karibu sana Kikwale Sekondari.


.....
STANSLAUS A. DANIEL
MKUU WA SHULE